4.	Installation of 2No. solar powered high mast flood lighting in Kipkelion East Constituency, Kericho County	MLPWHUD/SDHUD/SUD/346/2023-2024	Open
5.	Installation of 2No. solar powered high mast flood lighting in Funyula Constituency, Kakamega County	MLPWHUD/SDHUD/SUD/347/2023-2024	Open
6.	Installation of 2No. high mast flood lighting in Buura Constituency, Tana River County	MLPWHUD/SDHUD/SUD/348/2023-2024	Open
7.	Installation of 3No. Solar powered high mast at Mukothima, Gatunga and Kibung'a Markets in Tharaka Constituency, Tharaka Nithi County	MLPWHUD/SDHUD/SUD/349/2023-2024	Open
8.	Installation of 3No. solar powered high mast flood lighting in various centers in Rongo Constituency, Migori County	MLPWHUD/SDHUD/SUD/350/2023-2024	Open
9.	Installation of 2No. Solar Powered High Mast Floodlights in Suba South Constituency, Homabay County	MLPWHUD/SDHUD/SUD/351/2023-2024	Open
10.	Installation of 2No. Solar Powered High Mast Floodlights at Kawangware Day and Congo Roundabout in Dagoretti North Constituency, Nairobi County	MLPWHUD/SDHUD/SUD/352/2023-2024	Open
11.	Installation of 2No. Solar Powered High Mast Floodlights at Ngoingwa Thika west and Munyu Thika East in Thika town Constituency, Kiambu County	MLPWHUD/SDHUD/SUD/353/2023-2024	Open
12.	Installation of 2No. Solar Powered High Mast Floodlights at Mpaka and Lirhembe Markets, Ikolomani Constituency, Kakamega County	MLPWHUD/SDHUD/SUD/354/2023-2024	Open
13.	Installation of 2No. solar powered high mast flood lighting in Kuria East Constituency, Migori County	MLPWHUD/SDHUD/SUD/355/2023-2024	Open
14.	Installation of 2No. solar powered high mast flood lighting in Suba North Constituency, Homabay County	MLPWHUD/SDHUD/SUD/356/2023-2024	Open
15.	Installation of 3No. solar powered high mast flood lighting in Ruiru Constituency, Kiambu County	MLPWHUD/SDHUD/SUD/357/2023-2024	Open
16.	Installation of 2No. solar powered high mast flood lighting in Homa Bay Town Constituency, Homabay County	MLPWHUD/SDHUD/SUD/358/2023-2024	Open
17.	Installation of 2No. solar powered high mast flood lighting in Emgwen Constituency, Nandi County	MLPWHUD/SDHUD/SUD/359/2023-2024	Open
18.	Installation of 2No. solar powered high mast flood lighting in Gatundu North Constituency, Kiambu County	MLPWHUD/SDHUD/SUD/360/2023-2024	Open
19.	Installation of 4No. solar powered high mast flood lighting at Kwavonza, Kusyani kwakikului and Nthongoni in Kitui Rural, Kitui County	MLPWHUD/SDHUD/SUD/361/2023-2024	Open
20.	Installation of 2No. solar powered high mast flood lighting at Gagra Market and Asembo Bay market in Rarieda Constituency	MLPWHUD/SDHUD/SUD/362/2023-2024	Open
21.	Installation of 2No. solar powered high mast flood lighting at Kathemboni and Kameo in Machakos County	MLPWHUD/SDHUD/SUD/363/2023-2024	Open
22.	Installation of 2No. solar powered high mast flood lighting at Lusumu and Bunyala in Navakholo Constituency, Kakamega County	MLPWHUD/SDHUD/SUD/364/2023-2024	Open
23.	Installation of 1No. solar powered high mast flood lighting in Kipkeikei, Trans Nzoia County	MLPWHUD/SDHUD/SUD/365/2023-2024	Open
24.	Proposed construction of 2 No. Eco – Toilets at Shauri Yako, Manyatta, Embu County	MLPWHUD/SDHUD/SUD/366/2023-2024	Open
25.	Proposed Construction of Bondeni Market and Supporting Facilities, Migori County	MLPWHUD/SDHUD/SUD/367/2023-2024	Open
26.	Proposed Construction of Market Shed and Supporting Facilities and Drilling of Borehole, Trans Nzoia County	MLPWHUD/SDHUD/SUD/368/2023-2024	Open
27.	Proposed Construction of Market Shed and Supporting Facilities in Piny Oyier, Suna West Constituency, Migori County	MLPWHUD/SDHUD/SUD/369/2023-2024	Open
28.	Proposed Construction of Oyani Maasai Market Shed and Supporting Facilities, Migori County	MLPWHUD/SDHUD/SUD/370/2023-2024	Open
29.	Proposed Upgrading to Cabro Standards of 700M Sikunanga Access Road, Kesses Constituency, Uasin Gishu County	MLPWHUD/SDHUD/SUD/371/2023-2024	Open
30.	Proposed Upgrading to Cabro Standards of 500M Kathita Access Road, Manyatta Constituency, Embu County	MLPWHUD/SDHUD/SUD/372/2023-2024	Open
31.	Proposed Upgrading to Cabro Standards of 800M Access Roads – Karuri market Access Road and Kihara Modern Market Access Road in Kiambaa Constituency, Kiambu County	MLPWHUD/SDHUD/SUD/373/2023-2024	Open
32.	Proposed Upgrading to Bitumen Standards of 500M Access Road and Recarpeting of Existing 600M Road at Mukuyu Market, Kiharu Constituency, Muranga County	MLPWHUD/SDHUD/SUD/374/2023-2024	Open
33.	Proposed Construction of Changamwe Youth Center, Changamwe Constituency Mombasa County	MLPWHUD/SDHUD/SUD/375/2023-2024	Open
34.	Proposed construction of water reticulation system in Timau informal settlement phase 2, Meru County	MLPWHUD/SDHUD/SUD/376/2023-2024	Open
35.	Proposed Additional Works in Bondeni Market Kitale, Trans- Nzoia County	MLPWHUD/SDHUD/SUD/377/2023-2024	Open
36.	Proposed Installation of solar street Lights in Watamu, Kilifi North - Kilifi County	MLPWHUD/SDHUD/SUD/379/2023-2024	Open
37.	Proposed Construction of Social Housing and Associated Infrastructure at Kibra Constituency, Nairobi County	MLPWHUD/SDHUD/SUD/380/2023-2024	Open
38.	Proposed construction of Social Housing units at Michinda Boys' Primary School in Elburgon, Molo Constituency, Nakuru County	MLPWHUD/SDHUD/SUD/381/2023-2024	Open
39.	Proposed Construction of Social Housing and Associated Infrastructure in Kibra Constituency, Nairobi County (Lot 1, Lot 2, Lot 3, Lot 4, Lot 5)	MLPWHUD/SDHUD/SUD/382/2023-2024	Open
40.	Proposed Construction of Social Housing and Associated Infrastructure in Mathare constituency, Nairobi County (Lot 1, Lot 2)	MLPWHUD/SDHUD/SUD/383/2023-2024	Open
41.	Proposed Construction of Social Housing and Associated Infrastructure in Mathare 2 Constituency, Nairobi County (Lot 1, Lot 2)	MLPWHUD/SDHUD/SUD/384/2023-2024	Open
42.	Proposed Construction of Social Housing and Associated Infrastructure in Kasarani constituency Nairobi County (Lot 1, Lot 2, Lot3, Lot 4)	MLPWHUD/SDHUD/SUD/385/2023-2024	Open
43.	Proposed Construction of Social Housing and Associated Infrastructure in Kamiti, Kiambaa Constituency, Kiambu County (Lot 1, Lot 2)	MLPWHUD/SDHUD/SUD/387/2023-2024	Open
44.	Proposed Construction of Social Housing and Associated Infrastructure in Mariguini, Nairobi County	MLPWHUD/SDHUD/SUD/388/2023-2024	Open
45.	Proposed Construction of Infills at Mavoko SNP, Mavoko Constituency, Machakos County	MLPWHUD/SDHUD/SUD/389/2023-2024	Open
46.	Proposed Construction of Box Culvert and Remedial Works at Kibera Soweto, Nairobi County	MLPWHUD/SDHUD/SUD/390/2023-2024	Open

1. Interested bidders can access the tender document from the State Department's website www.housingandurban.go.ke free of charge. Bidders may download the tender documents from the website and are required to provide their details by registering with the Supply Chain Management Office, located at Ardhi House 6th Floor Wing B, 1st Ngong Avenue, during normal working hours. All enquiries and clarifications should be sent via email to: procurement@housingandurban.go.ke.

2. Qualified and interested Tenderers may obtain further information and inspect the Tender Documents during office hours between 8:00am-5:00pm at the address given below.

3. Tenders shall be quoted in Kenya Shillings and shall include all taxes. Tenders shall remain valid for 120 days from the date of opening of tenders.

4. Completed tenders must be delivered to the address below on or before **Tuesday, before 31st May, 2024 at 9:00am**. Electronic Tenders will not be permitted.

5. Tenders will be opened immediately after the deadline date and time specified above or any deadline date and time specified later. Tenders will be publicly opened in the presence of the Tenderers' designated representatives who choose to attend at the address below.

6. Late tenders shall be rejected.

7. The addresses referred to above are:

Head Supply Chain Management Service
For: The Principal Secretary
State Department for Housing and Urban Development.
P.O. Box 30119 -00100
NAIROBI, KENYA



Chuo Kikuu cha Egerton chatoa ardhi, utaalamu katika ulinzi wa ardhi ya kinamasi kwa NEMA

NA ESTHER MWANGI
(KNA)


Chuo Kikuu cha Egerton kinashirikiana na Mamlaka ya Kitaifa ya Kusimamia Mazingira (NEMA) kulinda na kurejesha vyanzo vya maji katika Kaunti ya Nakuru na kuzuia vitisho zaidi vina vyosababishwa na shughuli za kibinadamu.

Naibu Chansela wa Chuo hicho, Prof Isaac Kibwage, alisema kuwa taasisi hizo zinapanga kuingia katika Mkataba wa Maelewano ili kurejesha mali muhimu ya ikolojia, ikiwa ni pamoja na eneo la Msitu wa Keringet na Bwawa la Kenyatta ndani ya Kaunti ya Nakuru.

Akifichua dhamira ya chuo kikuu ya kutoa ekari ya ardhi ndani ya bewa lake kuu la Njoro kwa mipango ya upanzi wa miti wa NEMA, Prof Kibwage alieleza kuwa uvamizi kwa shughuli za kilimo, uchafuzi wa mazingira, ukuaji wa miji na mabadiliko ya hali ya hewa, miongoni mwa mengine, ni tishio kuu kwa vyanzo vya maji Kenya.

Mhadhiri huyo aliongeza kuwa hii imesababisha kutoweka kwa vyanzo vya maji muhimu na bidhaa na huduma zinazohusiana.

Akizungumza alipokaribisha ujumbe ulioongozwa na Mwanachama wa Bodi ya NEMA Prof



Naibu Chansela wa Egerton Prof Isaac Kibwage (Kulia) na mjumbe wa Bodi ya NEMA Prof. Charles Ngome, walipoanzisha ushirikiano wa kulinda na kurejesha ya kinamasi katika Kaunti ya Nakuru na kuzuia vitisho zaidi vinavyotokana na shughuli za kibinadamu.

Charles Ngome, Naibu wa Chansela alitaja michango ya Chuo Kikuu cha Egerton katika urejeshaji wa chemchemi za maji, ikiwa ni pamoja na Mto Njoro.

Taasisi hiyo ambayo pia ilizindua uchomaji taka za plastiki katika chuo kikuu mnamo 2017, imeandaa makala tisa mfululizo ya mbio za kukusanya pesa kuhifadhi msitu wa Mau na imeunda bustani ya mimea.

“Shughuli za Klabu cha Mazingira cha Chuo Kikuu cha

Ardhi ya kinamasi ni muhimu kwa uhifadhi wa viumbe hai.

Egerton na michango ya kila mwaka ya miti huchangia katika uhifadhi wa mazingira. Mifumo ikolojia muhimu, mara nyingi haithaminiwi na haijatambuliwa,” alisema.

Prof Ngome alianadamana na Mkurugenzi wa Mazingira wa Eneo la Bonde la Ufa Bi Njoki Mukiri na Mkurugenzi wa NEMA Kaunti ya Nakuru Joseph Kopejo.

Walibainisha kuwa maeneo oevu ni maeneo yenye maji mengi, ambayo yanaweza kujumuisha mabwawa na vinamasi. Ni makazi muhimu kwa spishi nyingi za mimea na wanyama.

Zaidi ya hayo, maeneo hayo ni muhimu kwa uhifadhi wa viumbe hai.

Yanatoa makazi muhimu kwa ndege wanaohama, samaki na wanyamapori wengine.

Ardhi oevu pia ni muhimu kuhifadhi kaboni, yana uwezo wa kuhifadhi kiasi kikubwa cha kaboni kwenye udongo na mimea.

Alisema kwa kuhifadhi na kurejesha maeneo hayo, nchi inaweza ku-

saidia kupunguza uzalishaji wa gesi chafu na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Naibu Chansela aliwaitaka maafisa wa NEMA kusaidia kukomesha mikaratusi kupandwa kando ya mito, akisema watu wanapaswa kupanda miti ya kiasili na kuacha kulima mita 30 karibu na vyanzo vya maji na mae-

neo oevu.

Kulingana na Shifika la Mazingira la Umoja wa Mataifa, maeneo oevu ni miongoni mwa mifumo ikolojia muhimu zaidi duniani, ikitoa huduma mbalimbali za mfumo ikolojia.

Hizi ni pamoja na uhabiti wa mafuriko, kusafisha maji na kudhibiti hali ya hewa.



MINISTRY OF MINING, BLUE ECONOMY AND MARITIME AFFAIRS

State Department for Blue Economy & Fisheries



Kenya Marine Fisheries and Socio-Economic Development Project (KEMFSED)
P O Box 58187 - 00200 NAIROBI

Request for Expression of Interest

(Procurement Specialist-NPCU - Individual Selection)

Country	Kenya
Name of project:	Kenya Marine Fisheries and Socio-Economic Development Project (KEMFSED)
Project No.:	P163980
Credit No.:	65400-KE
PROCUREMENT/CONTRACT REF NO.:	KE-MOMBEMA-C3-2023-028-ICS-INDV/MMBE&MA/SDBE&F/29/2023-2024

This Request for Expression of Interest follows the General Procurement Notice for this project that appeared in Development Business of 10th August 2020.

The Government of Kenya has received a Credit World Bank towards the cost of the Kenya Marine Fisheries and Socio-Economic Development Project (KEMFSED) and intends to apply part of the proceeds for consulting services for Procurement Specialist.

The consulting services (“Services”) include the assignments of Procurement Consultant as detailed in the TOR. The detailed Terms of Reference (TOR) for the assignments can be found at the following website: www.kemfsed.org, www.mibema.go.ke, and www.tenders.go.ke

The Services Contracts is expected to be for period 12 Months.

The State Department of Blue Economy and Fisheries (the “Client”) through the Kenya Marine Fisheries and Socio-Economic Development (KEMFSED) Project now invites individuals (“Consultants”) to indicate their interest in providing the Services. Interested Consultants should provide information demonstrating that they have the required qualifications and relevant experience to perform the Services. Interested individuals must provide information indicating that they are qualified to perform the services (attach curriculum vitae (CV), copies of documentary evidence of academic qualifications, professional qualifications, and registration/licensing with professional bodies). The shortlisting criteria is detailed in TOR.

The attention of interested Consultants is drawn to Section III, paragraphs, 3.14, 3.16, and 3.17 of the World Bank’s “Procurement Regulations for IPF Borrowers” first published July 2016 and revised September 2023, fifth edition (“Procurement Regulations”), setting forth the World Bank’s policy on conflict of interest.

An Individual Consultant will be selected in accordance with the Selection of Individual Consultants method set out in the Procurement Regulations.

Further information can be obtained at the address below from 0900 to 1700 hours East African Time (EAT) from Monday to Friday excluding lunch hour (1300 to 1400hours EAT) and public holidays.

Expression of interest must be delivered by 28th May 2024 at 1100hours EAT, using one of the following modalities: (i) Deposit in the tender box located on Mezzanine Floor, Maktaba Kuu Building Opposite NHIF Ngong Road Nairobi, Kenya or (ii) Send by email to: info@kemfsed.org and quote the Procurement Specialist REF NO.:KE-MOMBEMA-C3-2023-028-ICS-INDV; MMBE&MA/SDBE&F/29/2023-2024 in the subject row. For expressions of interest that will be deposited at the tender box, the packages should be clearly marked Procurement Specialist REF NO.:KE-MOMBEMA-C3-2023-028-ICS-INDV; MMBE&MA/SDBE&F/29/2023-2024.

The address (es) referred to above is (are):

Physical Address	Other addresses
<p>The Principal Secretary Ministry of Mining, Blue Economy and Maritime Affairs State Department for Blue Economy and Fisheries Ngong Road, NHIF Building 13th Floor P O Box 58187 - 00200 NAIROBI Email: ps@blueeconomy.go.ke Website: https://www.mibema.go.ke;</p>	<p>The National Project Coordinator Kenya Marine Fisheries and Socio-Economic Development (KEMFSED) Project Ministry of Mining, Blue Economy and Maritime Affairs State Department for Blue Economy & Fisheries Maktaba Kuu Building, Mezzanine Floor, Ngong Road, www.kemfsed.org Email: info@kemfsed.org Telephone: +254-20-2718870</p>



NATIONAL OPEN TENDER NOTICE

The National Irrigation Authority (Authority) invites sealed tenders for the following:

S.No.	Tender No.	Tender Name	Tender Submission Deadline	Target Group
1.	NIA/T/257/2023-2024	Provision of Guarding, Alarms and Security Services for National Irrigation Authority for the period 1 st July 2024-30 th June 2025	27 th May 2024 at 12.00 noon local time	All

Detailed tender document that include mandatory preliminary requirements, technical and financial evaluation criteria may be viewed and obtained by interested and eligible tenderers free of charge from the Authority’s website: <http://www.irrigation.go.ke/tenders> or Public Procurement Information Portal: <https://tenders.go.ke/> as from 17th May 2024. Tenderers who intend to submit their tenders MUST promptly submit their names and contact details to purchasing@irrigation.go.ke or ceo@irrigation.go.ke for communication on any clarification(s) and addendum arising during the tendering process.

Physical Address
Chief Executive Officer/CEO
National Irrigation Authority (NIA)
Irrigation House,
Lenana Road, Hurlingham, Nairobi, Kenya
Tel: +254-711061000
E-mail: ceo@irrigation.go.ke; purchasing@irrigation.go.ke

CHIEF EXECUTIVE OFFICER/CEO
NATIONAL IRRIGATION AUTHORITY

Maafisa wa afya ya umma watumwa mafuriko yakiathiri maeneo mengi

NA JOSEPH NG'ANG'A
(KNA)

Serikali imesambaza jumla ya kilo 1,226,400 za vyakula muhimu vinavyojumuisha mchele na maharage kwa familia zilizoathiriwa na mafuriko yanayoendelea kote nchini. Msemaji wa serikali Isaac Mwaura alisema kuwa chakula hicho kilisambazwa kusaidia jamii zilizoathirika katika maeneo ya Busia, Homabay, Kisumu, Machakos, Makueni, Tana River, Kilifi, Nakuru, Garissa, Turkana, Isiolo, Migori, Kajiado, Nairobi, Nyandarua, Kiambu, na Kaunti za Muranga. Akizungumza jijini Nairobi alipokuwa akitoa taarifa kuhusu mafuriko yanayoendelea, Mwaura alisema kuwa maafisa 30 wa afya ya umma pia wametumwa kwa ajili ya kutathmini hatari ya kambi zote 167 za wakimbizi wa ndani na kutathmini maeneo salama ya maji ya kunywa, usafi wa mazingira na usafi (WASH). “Hali ya mafuriko inaendelea katika sehemu nyingi za nchi, huku utabiri wa hali ya hewa wa hivi punde ukionyesha kuwa mvua kubwa na ngurumo zitaendelea katika kaunti 31.”

Mikoa iliyoathirika ni pamoja na Bonde la Ziwa Victoria, Bonde la Ufa, Kanda ya Kati na



Msemaji wa serikali Dkt Isaac Mwaura alipokuwa akitoa vifaa muhimu kwa familia zilizoathiriwa na mafuriko. Picha kwa hisani.

Mashariki. Mvua za mara kwa mara pia zinatabiriwa Nairobi na kanda ya Pwani, na kuathiri Kaunti za Tana River, Kwale, Mombasa, Kilifi, Lamu,” Mwaura alisema. Aliongeza kuwa Ziwa Victoria na Ziwa Baringo zinatabiriwa kuendelea kusababisha mafuriko na mafuriko ya kata katika mabonde ya Ziwa Victoria na Ziwa Baringo. Zaidi ya hayo, Mwaura alisema mvua kubwa inayoendelea kunyesha katika Kanda ya Kati

na kufurika kwa Mabwawa ya Seven Forks, kunasababisha hatari ya kuongezeka kwa mafuriko katika Kaunti za Tana Delta na Garissa, Tana River na Lamu.

Hali hizi mbaya za hali ya hewa zinaendelea kuathiri sekta mbalimbali za uchumi wetu

“Hali hizi mbaya za hali ya hewa zinaendelea kuathiri sekta mbalimbali za uchumi wetu ikiwa ni pamoja na usafiri, nyumba, elimu, afya na kilimo. Vile vile tunahuzunishwa na kuongezeka kwa idadi ya vifo, na tunatuma rambirambi zetu za dhati kwa familia na marafiki walioathirika. “Hadi leo tunaomboleza vifo vya watu 257 huku watu wazima 14 na watoto watano wakiripotiwa kufariki ndani ya saa 24 zilizopita. Jumla

ya watu 188 wamejeruhiwa, huku watu 293, 661 wameathiriwa na kaya 54,837 wamelazimika kuyahama makazi yao,” Mwaura alisema. Alisema vituo 61 vya afya vimeathirika katika kaunti 11 na mazao kwenye takriban ekari 9,816 ya ardhi yameharibiwa. “Jumla ya visa 44 vya kipindupindu vimeripotiwa kufikia sasa, huku Wizara ya Afya pamoja na Shirika la Msalaba Mwekundu la Kenya zikiendesha programu za kufikia matibabu pamoja na kudhibiti kipindupindu na magonjwa mengine yanayosababishwa na maji katika Kaunti za Tana River na Marsabit,” Mwaura alisema. Msemaji wa Serikali alisema mafuriko hayo yana athari mbaya kwa njia za reli na uendeshaji wa treni. Hii inajumuisha sehemu kati ya Thika na Nanyuki na vile vile ndani ya sehemu ya reli ya Chemelil na Kibigori kwenye njia ya tawi la Nakuru-Kisumu. Operesheni za masafa marefu za Nairobi-Kisumu na Nairobi-Nanyuki pia zimeathirika kwani shughuli bado hazijarejelewa. Kazi za ukarabati zinaendelea kwa sasa, huku Mamlaka ya Reli ya Kenya ikilenga kufungua njia zilizoathirika kufikia mwisho wa Mei 2024. “Aidha, mabwawa 192 yametambuliwa kuwa hatarishi, kufuatia tathmini ya kitaifa ya mabwawa yote. Kwa hivyo, shughuli mbalimbali za kuwahamisha watu zi-

nafanywa kote nchini, kufuatia noti ya saa 24 ya kuwahamisha, ambayo ilianza kutumika tarehe 2 Mei, na ambayo ilitolewa kwa makazi katika kaunti 33 ambazo ziko ndani ya mabwawa 178 na mabwawa hatarishi na hifadhi za maji,” Mwaura alieleza. Alisema katika Kaunti ya Nairobi, kaya zinazoishi ndani ya barabara za mita 30 na vyanzo vingine vya maji, kwa sasa wanahamishwa kwa usalama wao na noti za uhamishaji pia zimetolewa kwa wakaazi wote katika maeneo yanayokumbwa na maporomoko ya ardhi na matope. “Zaidi, ilani zimetolewa kwa wale walio katika sehemu zilizo ndani ya njia za mifereji ya maji ya vichuguu vya reli ya Kenya, ili kutoa nafasi kwa ukarabati wa miundombinu ya reli,” Mwaura alisema.

Aliendelea, “Kuna shughuli nyingi za utafutaji na uokoaji ambazo zinaendelea nchini kote, kuwahamisha watu walioathiriwa hadi maeneo ya juu na kuzipa kaya zilizoathirika msaada wa matibabu na kuhusiana.” Mwaura aliongeza kuwa serikali za kaunti, Vikosi vya Ulinzi vya Kenya, Huduma ya Walinzi wa Pwani ya Kenya, Huduma ya Wanyamapori ya Kenya, na Shirika la Msalaba Mwekundu la Kenya zimeshughulikia dharura na kufanikiwa kuwahamisha wakaazi katika Kaunti za Kisumu, Narok, Machakos, Nakuru na Tana River.

Huduma ya Misitu ya Kenya yaungana na jeshi kupanda miti katika Kaunti ya Wajir

NA HAMDHI BUTHUL NA SHARMARKE HAIR(KNA)

Shirika la Huduma ya Misitu nchini (KFS) imeungana na Jeshi la Kenya kuongoza kampeni ya kupanda miti katika Kaunti ya Wajir ili kukabiliana na uharibifu wa mazingira na kuimarisha uendelevu katika eneo hilo Kame na Nusu Kame. Mpango huo uliozinduliwa huku mvua ikiendelea kunyesha kwa muda mrefu, unalenga kuchangia katika lengo kuu la serikali la kufikia asilimia 30 ya miti kote nchini. Akizungumza baada ya zoezi la upanzi wa miti katika Wajir Airbase, Mkuu wa Huduma ya Misitu nchini Kenya katika kanda hiyo, Bi Ambiya Osman alisisitiza jukumu muhimu la kupanda miti katika kupunguza athari za

kuongezeka la joto duniani. Bi Osman alisisitiza kwamba kwa kuondoa kaboni na kutoa oksijeni, miti ina jukumu muhimu katika kurejesha uwiano wa kiikolojia.

Bi Osman aliwataka watu binafsi kuukubali mpango huo kama jukumu la kibinafsi, akionyesha umuhimu wake katika kupata mustakabali endelevu kwa vizazi vijavyo.

Brigedia David Chesire, Kamanda wa Kanda ya Kaskazini Mashariki, aliunga mkono maoni ya Bi Osman, akisisitiza umuhimu wa kutunza miche iliyopandwa.

Chesire aliwataka wananchi kutoa huduma ya mara kwa mara ikiwa ni pamoja na kumwagilia maji wakati wa kiangazi na ufuatiliaji makini wa wadudu na magonjwa.

Chesire aliendelea ku-sisitiza juhudi za pamoja zinazohitajika ili kuhakikisha mafanikio ya jitihada hizo, akisisitiza kwamba hata hatua ndogo zinaweza kutoa matokeo muhimu katika kujenga kesho bora.

Mvua inayoendelea kunyesha ilitambuliwa kama msaada kwa miti mipya iliyopandwa, kutoa umwagiliaji wa asili na kukuza ukuaji wa mizizi. Hali hii nzuri ya hali ya hewa hutoa mwanzo mzuri kwa miche, kuweka hatua ya ukuaji. Mpango huo unajiri kukiwa na changamoto za mazingira katika Kaunti ya Wajir, kama ilivyoangaziwa na ripoti ya hivi majuzi ya tathmini iliyofanywa na Chama cha Msalaba Mwekundu (KRCS) na washirika wengine.

Waziri asisitiza umuhimu kupanda miti kudhibiti mabadiliko ya tabianchi

NA MWANDISHI WA MYGOV

Waziri wa Mpango ya Kiuchumi na Hazina ya Kitaifa, Prof Njuguna Ndung'u, alisisitiza umuhimu wa upanzi wa miti kote nchini kama hatua muhimu ya kukabiliana na mabadiliko ya hali ya hewa.

Akizungumza katika Msitu wa Mumandu katika Kaunti ya Machakos, Prof Ndung'u, ambaye alikuwa mgeni rasmi wakati wa Zoezi la Kitaifa la Kupanda Miti lililofanywa kote nchini, alisisitiza umuhimu wa zoezi la kupanda miti katika kukabiliana na changamoto inayojitokeza kimataifa ya mabadiliko ya hali ya anga.

Waziri huyo aliyeadamana na Gavana wa Machakos Bi Wavinya Ndeti na viongozi wengine mashuhuri, alisisitiza

umuhimu wa mpango huo katika kulinda afya na uthabiti wa sayari kwa vizazi vijavyo.

Ndung'u alisisitiza kuwa upanzi wa miti unaendana na juhudi za kitaifa na kimataifa za kukabiliana na mabadiliko ya hali ya hewa na kuimarisha misitu, na alitumia hafla hiyo kuanziza majanga matatu yanayowakabili wanadamu-mabadiliko ya hali ya hewa, kupotea kwa asili, na uchafuzi wa mazingira.

“Hivi majuzi Kenya iki-kumbwa na ukame mbaya zaidi katika miongo minne, na kusababisha hasara ya zaidi ya mifugo milioni 2.5 na kuathiri moja kwa moja maisha ya Wakenya zaidi ya milioni nne,” Waziri alisema.

Waziri huyo aliongeza kuwa hasara za kijamii na kiuchumi kutokana na mabadiliko ya hali

ya hewa katika muongo mmoja uliopita zimeathiri vibaya Pato la Taifa la Taifa (GDP).

Aidha, Prof alisema mvua kubwa inayoendelea kunyesha imesababisha mafuriko na uharibifu mkubwa na kuathiri sekta mbalimbali za uchumi ikiwemo kilimo, miundombinu na utalii na hivyo kukwamisha juhudi zetu za kufufua uchumi.

Zaidi ya hayo, Waziri alisema, Serikali inawekeza katika kuzalisha mbegu bora za miti, ikiongozwa na Taasisi ya Utafiti wa Misitu ya Kenya, na kutafuta fursa za kilimo mseto na ukuzaji wa matunda kama parachichi, maembe na makadamia.

Mipango hii, alisema, sio tu kwamba inaunda fursa za kazi salamakwa mazingira lakini pia kufungua masoko mapya ya njie

Serikali kuunga Mswada unaopendekezwa wa Wakaguzi wa Ndani ili kuongeza ufanisi

BY MUTISO MBITHI
(MYGOV)

Waziri la Utumishi wa Umma, Moses Kuria, ameahidi serikali inaunga mkono Mswada wa Wakaguzi wa Ndani unaopendekezwa, ambao unanua kurahisisha utendakazi wa wakaguzi wa ndani nchini Kenya kwa kuongeza ufanisi.

“Nitashauriana na Prof Njuguna Ndung’u, Waziri wa Hazina ya Kitaifa, ili Mswada wa Wakaguzi wa Ndani uidhinishwe ili ifikapo Bungeni, kiongozi wa walio wengi awe na wakati rahisi kushawishi kupitishwa kwake,” Kuria alisema.

Mswada huo unalenga kuendeleza utekelezaji wa viwango na maadili mema katika taaluma ya ukaguzi wa ndani.

Pia unalenga kudhibiti ukaguzi unaofanywa na wakaguzi wa ndani, kuhakikisha udumishaji wa viwango vya ukaguzi wa ndani vinavyowiana na vya kimataifa, na kutoa taratibu za hatua za kinidhamu miongoni mwa wataalamu wa ukaguzi wa ndani.

Waziri Kuria alisema haya mjini Mombasa wakati wa Semina ya 21 ya Mwaka ya Ukaguzi wa Ndani. Semina hiyo ililenga uvumbuzi, faragha ya data, viwango vya ukaguzi wa ndani, hatari ya usimamizi na uzingatiaji, masuala ibuka, uongozi, na ukaguzi usio na makosa.

Katika semina hiyo pia alikuwepo Kimani Ichung’wah, Mbunge wa Kikuyu na kiongozi wa Wengi Bungeni, ambaye alibainisha kuwa nchi inategemea juhudi za vyombo vya kitaaluma kama vile Taasisi ya Wakaguzi wa Ndani (IIA) Kenya kuhakikisha wataalamu wanatekeleza viwango vya juu zaidi vya maadili ili kuimarisha uwazi na



Waziri wa Utumishi wa Umma, Utendaji na Usimamizi wa Uwasilishaji Moses Kuria (kulia) akiwa na Kimani Ichung’wah, Mbunge wa Kikuyu na kiongozi wa Wengi Bungeni (kushoto). Pamoja nao ni CPA Leonard Okoth, Mwenyekiti wa Taasisi ya Wakaguzi wa Ndani (Kenya) wakati wa Semina ya 21 ya Mwaka ya Ukaguzi wa Ndani mjini Mombasa.

uwajibikaji katika matumizi ya fedha za umma miongoni mwa mashirika ya sekta ya umma.

“Ninaalika uongozi wa IIA (Kenya) kufanya kazi na Bunge kuweka sheria zinazohakikisha wanachama wa Taasisi wanawajibika ili kuimarisha usimamizi wa taasisi zetu,” alisema Ichung’wah.

Kupitishwa kwa Mswada wa Ukaguzi wa Ndani kuwa Sheria kuhakikisha uhuru wa kazi za ukaguzi wa ndani katika mashirika yao. Pia, wanachama watapata vyeti vinavyohitajika ili kuongeza ujuzi wao katika ukaguzi wa ndani na kuhakikisha wanaweza kufanya kazi bila hofu ya kukemewa au kupoteza ajira zao.

Semina hiyo pia ilihudhuriwa na Ahmed Abdullahi, Makamu Mwenyekiti, Baraza la Magavana ambaye pia ni Gavana wa Wajir ambaye alisema ili kuimarisha ufanisi wa michakato ya

ukaguzi wa ndani katika serikali za kaunti, kamati za ukaguzi za kaunti zinapaswa kutoa usimamizi thabiti wa ripoti ya fedha, mchakato wa ukaguzi na mifumo ya udhibiti wa ndani pamoja na kufuata sheria na kanuni.

“Baraza la Magavana limeshirikiana na Bodi ya Viwango vya Uhasibu katika Sekta ya Umma ili kuimarisha upitishaji wa mifumo na miongozo ya wakaguzi wa ndani na kamati za ukaguzi katika serikali za kaunti katika azma ya kuimarisha ufanisi wa kazi za ukaguzi wa ndani,” Mohammad alisema.

Mwenyekiti wa IIA (Kenya), Leon-

Bila ushauri sahihi, nchi inaweza kufanya maamuzi ambayo hayana uungwaji mkono wa data

ard Okoth, alisema kuwa baadhi ya hatari kuu kwa Wakaguzi wa Ndani nchini Kenya na duniani kote ni pamoja na upatanishi wa malengo, uwezo wa kutambua hatari zinazojitokeza na uwezo wa kukabiliana na hali hiyo, mabadiliko ya ujuzi, mabadiliko ya matarajio ya thamani ya washikadau na teknolojia inayovuruga ikiwemo Akili Unde miongoni mwa zingine. Semina ya kila mwaka hufanyika Mei wakati wakaguzi wa ndani kote ulimwenguni wanasherehekea taaluma hiyo.

IIA (Kenya) inashirikiana na Taasisi ya Wakaguzi wa Ndani Inc. yenye makao yake makuu Florida, Amerika. IIA ni sauti ya kimataifa ya taaluma ya ukaguzi wa ndani. Wanachama hufanya kazi katika ukaguzi wa ndani, udhibiti wa hatari, utawala, udhibiti wa ndani, ukaguzi wa teknolojia ya habari, elimu na usalama.

Wanauchumi wahimizwa kutoa ushauri unaotegemea data

NA SADIK HASSAN (KNA)

Serikali inawataka wanauchumi kuunda ushauri unaotokana na data ili kuendeleza mageuzi ya kiuchumi nchini.

Katibu wa Masuala ya Baraza la Mawaziri Dkt Idris Dokota, ambaye alizungumza mjini Mombasa ambako wanachumi walikusanyika kwa Kongamano la Siku tano la Wanachumi lililoandaliwa na Jumuiya ya Wanachumi wa Kenya (ESK), alisisitiza kwamba wanauchumi wanapaswa kufafanua aina ya ushauri wanaotoa kwa data, kwani hizi ni muhimu katika kufanya maamuzi.

“Hii ndiyo njia ya pekee ambayo nchi itatumia kufanya maamuzi yanayotokana na data. Bila ya ushauri sahihi, nchi inaweza kufanya maamuzi ambayo hayategemei data, na hivyo kusababisha maamuzi ambayo tunayaita yasiyo sahihi katika masuala ya maendeleo ya kiuchumi,” Dkt Dokota alisema.

Katibu alisema ESK ndilo shirika kubwa zaidi la kitaaluma nchini na limetoa mchango mkubwa kwa kuzalisha wataalamu na hivyo ku-

changia mabadiliko ya nchi.

“Shirika hili linahitaji kukitwa katika sheria, mara linapoundwa kwa sheria ya bunge, basi tutaweza kuwa na nguvu na uhakika katika kile tunachofanya,” alisema.

Dkt Dokota, ambaye kitaalumu ni mwanachumi aliyebobea, aliwasilisha mada kuhusu athari za kutokuwa na uhakika wa kisiasa kwa mabadiliko ya hali ya hewa ambayo yamesababisha mafuriko, ukame wa muda mrefu, na kupungua kwa mazao.

“Hizi zimeweka vikwazo vya kusafirisha bidhaa nye ambapo nchi zimepiga marufuku usafirishaji wa bidhaa fulani ili ziweze kulinda akiba ya chakula na utoshelevu wa chakula,” alifafanua.

Katibu alisema kuwa kutokuwa na uhakika wa hali ya kisiasa katika baadhi ya maeneo kumesababisha ghasia na kuathiri uchumi wa dunia. Alisema ni wakati mwafaka kwa wanachumi kuja na mabadiliko ya kimuundo katika sera, na mfumo wa kisheria na udhibiti ili kukabiliana na matatizo yanayosababishwa na kutokuwa na uhakika.



Katibu wa Masuala ya Baraza la Mawaziri Dkt. Idris Dokota akiwahutubia Wanauchumi katika Kongamano la Wanauchumi mjini Mombasa.

Wajir yachukua hatua kulinda watoto na changamoto za hali ya hewa

NA HAMDI BUTHUL
(KNA)

Serikali ya Kaunti ya Wajir imejitolea kuwalinda watoto wakati wa hali mbaya ya anga nchini.

Ili kufanikisha hili, Idara ya Huduma kwa Watoto ya kaunti imeandaa mkutano muhimu, unaoangazia kuimarisha hatua za ulinzi wa watoto

katika kukabiliana na dharura za mafuriko.

Mratibu wa Kaunti ya Huduma za Watoto, Jillo Roba, alisisitiza hitaji muhimu la kujiandaa, kuitikia na mikakati ya uokoaji.

Alisema kaunti hiyo huwa katika hatari ya kukabiliwa na dharura, kuanzia ukame wa mara kwa mara hadi majanga ya

asili na yanayosababishwa na wanadamu.

Akieleza kuhusu uharibifu uliosababishwa na mafuriko makubwa ya Oktoba, Novemba, na Desemba 2023, Roba alisisitiza umuhimu wa dharura wa kutanguliza juhudi za ulinzi wa watoto.

Alisema kupoteza maisha, uharibifu wa mali, na watu kuhama makazi

yao kulisisitiza umuhimu wa kuchukua hatua madhubuti, na kuongeza, “Hatuwezi kumudu kusubiri majanga yatokee kabla ya kuchukua hatua,” Roba alisema.

Aliongeza kwamba, “Kukiwa na onyo la mapema ya mafuriko, ni muhimu kujiandaa vya kutosha kusaidia watu wetu.”

Akihutubia washikadau kutoka sekta mbalimbali katika mkutano wa dharura wa ulinzi wa watoto uliofanyika katika hoteli ya Wajir, mratibu huyo alieleza mipango ya kina inayolenga kujumuisha awamu za kabla, wakati, na baada ya dharura.

Roba alikariri kujitolea kutafuta pesa, kuhusisha washirika na kuongeza

uhamasishaji miongoni mwa wakazi ili kuimarisha ustahimilivu wa kaunti.

Naibu Kamishna wa Kaunti ya Wajir Magharibi, Kefa Kigeni, anayewakilisha Kamishna wa Kaunti hiyo, aliunga mkono maoni ya Roba, akisisitiza kuhusu athari za majanga kwa watoto, wazee na walio hatarini.

KenGen yapata idhini ya mtambo wa Sola PV katika Mabwawa ya Seven Forks

NA CHRIS MAHANDARA (KNA)

Kampuni ya Kuzalisha Umeme ya Kenya (KenGen) imepata idhini ya kuanzisha mtambo wa PV wa umeme wa Megawati 42.5 katika Mabwawa ya Seven Forks ili kuongeza uzalishaji wa umeme nchini.

Kupitia mpango huu, KenGen inalenga kutumia nguvu ya jua wakati wa mchana kuzalisha nguvu na kuhifadhi maji katika mabwawa makubwa ya kuzalisha umeme kuzalisha umeme usiku.

Mkurugenzi Mkuu wa KenGen, Mhandisi Peter Njenga, alisema kuwa mradi hautaongeza kiasi cha umeme kitaifa lakini pia utahakikisha usambazaji thabiti wa umeme ili kuchochea maendeleo ya kiuchumi.

Mhandisi Njenga aliongeza kuwa idhini zote za mradi huo zimekamiliwa, na hivyo kufungua njia kwa awamu ya ujenzi, ambayo itaanza hivi karibuni.

Akizungumza wakati wa Semina ya 12 ya KenGen mjini Kisumu, Mkurugenzi Mkuu alisisitiza kuwa mradi huo mpya unaashiria kuji-



Mkurugenzi Mkuu wa KenGen (MD) Eng. Peter Njenga (katikati) akihutubia wanahabari mjini Kisumu. Anayetazama ni Mwenyekiti wa Bodi ya KenGen Julius Ogamba (kulia).

tolea kwa kampuni katika uvumbuzi na kukumbatia nishati mbadala ili kukidhi mahitaji ya nishati nchini.

KenGen, aliongeza, inaanzisha miradi mingine kadhaa ili kuongeza rasilimali zilizopo ili kuleta utulivu wa uzalishaji wa umeme na kutoa umeme wa bei nafuu na wa ushindani kwa Wakenya.

Alitoa mfano wa Kituo cha Umeme cha Gogo katika Kaunti ya Migori ambacho kinaboreshwa kutoka megawati 2 ya sasa

hadhi megawati 8.6. "Hiki ni mojawapo ya vituo vyetu muhimu vya KenGen kwa sasa kwani kinabeba ahadi ya ukuaji wetu wakati ambapo upanuzi wa uwezo ulionekana kuwa hauwezekani," alisema.

KenGen, aliongeza, ilikuwa ikitumia mvua zinazoendelea kunyesha, kuongeza uzalishaji wa umeme wa maji ili kuhakikisha umeme zaidi unapatikana kwa Wakenya.

"Hapa kanda ya Magharibi, tumeongeza uzalishaji

wa umeme wa maji katika vituo vya Sondu na Sangoro pamoja na Turkwel kutokana na kuongezeka kwa mvua," alisema.

Mabwawa yaliyo chini ya usimamizi wa KenGen, alisema, yamesaidia kupunguza athari za mafuriko, haswa chini ya mkondo wa Mto Tana.

Mabwawa ya kuzalisha umeme katika eneo la Seven Forks, alisema yamefikia uwezo kamili wa usambazaji.

"Hii ina maana kwamba Mabwawa yetu ya Forks Saba yanashikilia sehemu kubwa ya maji yanayotiririka kutoka Mto Tana, ambayo yangefurika maeneo ya chini ya mabwawa hivyo kupunguza uharibifu unaosababishwa na mvua inayoendelea kunyesha," alisema.

Bwawa la Turkwel hata hivyo, alifichua, liko mbali na kufikia kiwango chake juu akisema hakuna sababu ya hofu kwa wale wanaoishi karibu na bwawa hilo.

"Hivi tunavyozungumza, kiwango cha bwawa ni mbali na kufikia kiwango cha juu cha mita 1,150, tuko mita 1,136," alisema.

KWA UFUPI

Mke wa Rais Rachel Ruto atoa misaada kwa waathiriwa wa mafuriko

Zaidi ya familia 800 zilizoathiriwa na mafuriko huko Kitengela, Kaunti ya Kajiado, zimepokea misaada wa chakula na vifaa vya nyumbani kupitia Afisi ya Mke wa Rais.

Mke wa Rais, Rachel Ruto, aliongoza zoezi la kusambaza misaada hiyo, kwa hisani ya serikali ya kitaifa, Wakfu wa Chandaria, na Hospitali ya Chuo Kikuu cha Aga Khan.

Mke wa Rais alikariri kujitolea kwa serikali kuwapa makazi Wakenya walioathiriwa na mafuriko yanayoendelea kote nchini.

Alibainisha kuwa mvua hiyo ilisababisha watu wengi kuyahama makazi yao, na kuwaacha bila chakula na malazi, na kuwataka watu wengine wenye nia njema kujitokeza na kuwasaidia walioathirika kwa njia yoyote ile. "Tunafahamu kuwa mvua inayoendelea kunyesha imeathiri familia nyingi, na tunajitahidi kuhakikisha kwamba walioathirika wanapata chakula na makazi," Bi Ruto alisema.

Gavana wa Kajiado Joseph

Ole Lenku alitoa wito kwa wakazi wanaoishi katika maeneo tambarare ambayo huathirika na mafuriko kuhama maeneo salama.

Ole Lenku alisema mvua hiyo kubwa imekatiza barabara na kusomba madaraja katika maeneo mengi ya kaunti hiyo huku Wadi ya Magadi ikiathirika zaidi.

Aliishukuru serikali ya kitaifa kwa hatua ya haraka ya kusaidia Wakenya ambao barabara zao zimekatizwa na mafuriko katika eneo la Magadi.

"Mvua imeathiri familia nyingi kutokana na madaraja kusombwa na maji katika baadhi ya maeneo kama vile Magadi," alisema.

Viongozi wengine wali-ohudhuria hafla hiyo ni pamoja na Waziri, Wizarara ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, Maeneo Kame na Nusu Kame, na Maendeleo ya Kikanda Peninah Malonza, Mbunge wa Kajiado Mashariki Kakuta Mai Mai, seneta mteule Peris Tobiko na madiwani wa Bunge la Kaunti ya Kajiado. Na Rop Janet (KNA)

Kaunti ya Laikipia yapokea misaada kutoka Uholanzi kukarabati vyanzo vya maji

Serikali ya Uholanzi imeshirikiana na Kaunti ya Laikipia kushughulikia changamoto za mabadiliko ya hali ya hewa, ikiwemo ukarabati wa minara ya maji iliyoharibika.

Naibu Balozi wa Uholanzi nchini Kenya, Jolis Van Bommel, akizungumza na vyombo vya habari mjini Nanyuki siku ya Jumatano, alisema kuwa wana nia ya kusaidia mipango ya kukabiliana na hali ya hewa inayolenga kujenga ustahimilivu ndani ya jamii.

"Tuko hapa kujadili mabadiliko ya hali ya anga na, kupitia wafadhili wengine, kuhakikisha kwamba kwa ushirikiano na serikali ya Kaunti ya Laikipia, tunasaidia shughuli zinazoongozwa na jamii ili kuboresha hali na kujenga ustahimilivu," alisema Balozi.

Zaidi ya hayo, serikali ya Uholanzi ilitoa ruzuku ya Sh10 milioni kupitia Shirika la World Wide Fund for Nature (WWF)-Kenya, inayotarajiwa kutumiwa na kaunti nne: Laikipia, Meru, Isiolo, na Nyeri, ambazo ziko ndani ya bonde la Ewaso Ng'iro chini ya mpango wa Ufadhili wa Hatua za

Hali ya Hewa zinazoongozwa na kaunti.

Ruzuku hiyo itatumika zaidi kuimarisha usimamizi juumuishi wa rasilimali za maji kupitia mashirika ya jamii yaliyopangwa kama vile Vyama vya Watumiaji Rasilimali za Maji (WRUAs) na Vyama vya Misitu vya Jamii (CFAs) ndani ya bonde la Ewaso Ng'iro.

Naibu Gavana wa Laikipia Joshua Irungu alisema kuwa kukabiliana na mabadiliko ya hali ya anga kwa kupanda miti, ni muhimu ili kuepusha hali hiyo, na hivyo basi kushirikiana na wafadhili ni misaada mkubwa kwa kaunti.

"Mabadiliko ya hali ya hewa ni ya kutisha na tunaweza kuona jinsi mafuriko yanavyoathiri maisha, kwa hivyo, kwa mipango kama hii ya ufadhili kutoka kwa wafadhili wetu, ni misaada mkubwa kwa jamii," alisema gavana huyo.

Mratibu wa Ushirikiano wa Bonde la Ewaso Ng'iro eneo la Mlima Kenya Stanley Kirimi alihimiza ushirikiano kutoka kwa washikadau wote ili kuona jinsi wakazi wanaweza kufaidika na maliasili bila kuharibiwa. Na Muturi Mwangi (KNA)

Wadau wakusanyika Nairobi kushughulikia changamoto za afya ya udongo Afrika

NA BERNADETTE KHADULI (KNA)

Mkuu wa Mawaziri na Waziri wa Masuala ya Kigeni na Wakenya wanaoishi ng'ambo, Musalia Mudavadi, anasema kuna haja ya bara la Afrika kuunda mifumo ya uratibu ambapo washikadau wote watakaa meza moja na kuandaa mipango ya utekelezaji itakayoshughulikia masuala ya mbolea na afya ya udongo.

Mudavadi alisema masuala ya mbolea na afya ya udongo yanahusu maeneo tofauti, na hivyo akawataka washikadau wote kujadiliana na kupata suluhu mwafaka na za kudumu.

Musalia, ambaye alikuwa akizungumza wakati wa Mkutano wa Pili wa Afrika wa Afya ya Mbolea na Udongo (AFSH) uliofanyika katika Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Kenyatta jijini Nairobi, pia aliwataka



Franklin Linturi, Waziri wa Kilimo na Maendeleo ya Mifugo, Kenya, Musalia Mudavadi, Katibu Mkuu wa Baraza la Mawaziri na Waziri wa Masuala ya Kigeni na Diaspora, Kenya, Amb. Kamishna wa Kilimo, Maendeleo Vijijini, Uchumi wa Bluu na Mazingira Endelevu wa Umoja wa Afrika, Joseph Sacko na Waziri wa Kilimo, Viwanda vya Wanyama na Uvuvi wa Jamhuri ya Uganda, Frank Kagyigy Tumwebaze wakiwa katika picha ya pamoja jijini Nairobi.

washiriki wa mkutano huo kubuni mapendekezo ya ufadhili ambayo yanayoweza kufikiwa, na kuongeza, "Hii ni njia ya pekee ya kufikia

malengo yaliyowekwa katika mipango kazi uchumi unapoimarika," alisema.

Hafla hiyo ya siku tatu, iliyoandaliwa na serikali

ya Kenya kwa ushirikiano na Umoja wa Afrika (AU), ilileta pamoja zaidi ya wadau 2,000 kutoka barani kote ili kutathmini hali ya afya ya udongo barani Afrika, mtandao kuhusu jinsi masuala bora yanayoathiri kilimo yanavyoweza kushughulikiwa na biashara katika hafla hiyo yenye mada "Sikiliza Ardhi".

Katika Azimio la Maputo la Julai 2003, Wakuu wa Nchi na Serikali waliidhinisha dhamira ya ugawaji wa angalau asilimia 10 ya rasilimali za bajeti ya kitaifa kwa kilimo na utekelezaji wa sera ya maendeleo maeneo ya mashambani ndani ya miaka mitano. Mkutano wa AFSH, kongamano kubwa zaidi la afya ya udongo barani, uliongozwa na Rais William Ruto na kusimamamiwa na Mwenyekiti wa Tume ya Umoja wa Afrika (AUC) Moussa Faki Mahamat.